COMPETECE BASED CURRICULUM
HOMEWORKK ENGAGEMENT ACTIVITY
LIKIZO YA DISEMBA
GREDI YA NNE

KISWAHILI

SEHEMU YA A: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Jibu maswali kwa kutamka (Alama 5)

1. *Ni nini wingi wa neno daftari?*
2. *Bendera yetu ina rangi ngapi?*
3. *Eleza maana ya "kutiwa nguvani"*
4. *Kamilisha methali ifuatayo, "Asiyesikia la mkuu....*
5. *Taja vazi moja la kike unalolijua.*

KUSOMA KWA SAUTI

Soma kifungu hiki kwa sauti (Alama 10)

Shule yetu inaitwa Bidii Jumanne ilikuwa ni siku ya sherehe ya kutia zawadi. Walimu wetu waliwasili mapema kwa matayarisho. Mgeni wetu wa heshima alipowasili, alipewa shada la maua. Shehe na kasisi walituombea kabla ya kuanza sherehe. Wanafunzi thelathini wa gredi ya nne walituzwa. Shangazi yangu alihudhuria kwa naiba ya mama yangu. Thuluthi mbili ya watu ambao walihudhuria walikuwa kina mama.

SEHEMU YA B: SARUFI

Andika visawe vya maneno yafuatayo

1. *Tembo*
2. *Nyanya*
3. *Jogoo*
4. *Barua*
5. *Motokaa*

Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendwa.

6. *Chora*
7. *osha*
8. *tuma*
9. *panga*
10. *lipa*

Unganisha sentensi kuwa joja kwa kutumia kiunganishi sahihi

11. *Alitekwa nyara. Hakudhulumiwa*
12. *Maria amevaa koti. Maria anahisi baridi*
13. *Utavaa jaketi. Utavaa koti*
14. *Nilienda katika kituo cha mabasi. Nilisafiri Lamu*
15. *Juma hakuvaa mlapa. Juma hakuvaa daluga*

Taja majina ya heshima unayotumia kuwaita wafuatao.